**MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WA WILAYA YA GUCHA KUSINI**
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
**KISWAHILI**
Karatasi ya Kwanza
(INSHA)
**Julai /Agosti 2016**
Muda: Saa 1¾

1. Andika barua kwa Mkurugenzi wa Elimu nchini ukimwelezea kuhusu mikakati inayostahili kuwekwa ili kupambana na tatizo la udanganyifu katika mitihani ya kitaifa.
2. Ukosefu wa ajira ni tatizo sugu humu nchini. Pendekeza njia zinazoweza kutumiwa katika kubuni nafasi tosha za kazi humu nchini.
3. Mjinga mpe kilemba utamwona mwendowe.
4. Anza kwa, "Walipofungua mlango huo, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Walilia kwi! kwi! kwi! kwa maafa waliyoshuhudia . . . ."

---

**MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA KUSINI**
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
**KISWAHILI 102/2**
Karatasi ya Pili
(Ufahamu, ufupisho, Sarufi na matumizi ya lugha na Isimujamii)
**Julai / Agosti 2016**
Muda: Saa 2½

**1. UFAHAMU (alama 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Utandaridhi (au globalization kwa lugha ya Kiingereza) ni jinsi ya maisha inayoendelea kutawala ulimwengu wote katika karne hii ya 21. Neno utandaridhi ni neno mseto ambalo maana yake ni utamaduni uliotanda au kuenea ardhi nzima. Mtu mtandaridhi hivyo basi ni mtu aliyebobea kikamilifu katika utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine. Mtandaridhi husisha sana katika kutandaridhi aina moja au nyingine ya **amara** muhimu za kitandaridhi. Hizo ni kama vile biashara za kimataifa, lugha za kimataifa, aina za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote, muziki wa kisiku hizi, hasa vile *pop, reggae, raga, rap*, ambao asili yake ya hivi majuzi ni Marekani. Muziki huo waimbaji wake hutumia, sana sana, lugha ya Kiingereza hususan kile cha Marekani na kadhalika. Watandaridhi wana nyenzo zingine kadha wa kadha za kuendeshea maisha yao au kujitambulisha. Wao huwasiliana kutoka pembe moja ya dunia hadi nyingine wakitumia vitumeme, yaani vyombo vitumiavyo umeme kufanya kazi ya hali ya juu, kama vile tarakilishi na simu, hata za mkono. Watu hawa hawakosi runinga sebuleni mwao, usiseme redio. Hawa husikiliza na kutazama habari za kimataifa kupitia mashirika matandaridhi ya habari kama vile BBC la Uingereza na CNN la Marekani. Aidha watu hawa husafiri mara kwa mara kwa ndege na vyombo vingine vya kasi. **Hawa hawana mipaka**. Wale wanaohusudu utandaridhi wanaamini kindakindaki kwamba utamaduni huu wa kilimwengu umeleta **mlahaka** mwema baina ya watu binafsi, makampuni makubwa makubwa ya kimataifa na uwiano bora baina ya mataifa. Watu hawa husikika wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni imeupigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimwenguni kote. Kwa upande mwingine, **wakereketwa** wa tamaduni za kimsingi za mataifa na makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandaridhi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo. Vile vile unaelekea kuangamiza lugha nyingi zilizofungamana na tamaduni hizo. Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umesemekena kwamba unasababisha kutovuka kwa utu miongoni mwa wanadamu wote, ambao wamo mbioni kusaka pesa na kuneemesha ubinafsi. Inadaiwa pia kwamba utandaridhi umesababisha kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huku kutovuka kwa adabu kwa vijana, hasa wale wa mataifa yanayojaribu kuendelea, kumeleta zahama **chungu mbovu**, ikiwa ni pamoja na kuenea kwa UKIMWI kwa kasi ya kutisha.

Maswali

a) i) Bainisha kwa kutoa maelezo kamili kwamba utandaridhi ni neno mseto. (alama 1)
   ii) Tohoa maneno mawili kutokana na neno kutandaridhisha kisha ueleze maana za maneno hayo. (alama 1)
b) i) Nini maana ya "hawa hawana mipaka"? (alama 1)
   ii) Kwa nini watandaridhi wanapenda kusikiliza na kutazama habari kupitia BBC na CNN? (alama2)
c) i) Eleza kikamilifu maoni ya watandaridhi kuhusu utamaduni wao. (alama 3)
   ii) Je, utandaridhi unalaumiwa kwa nini katika kifungu hiki? (alama 3)
d) Msemo : "chungu mbovu" ni msemo wa kimtaani tu. Msemo sawa ni upi? (alama 1)
e) Eleza maana ya maneno yafuatayo: (alama 3)
   i) amara .
   ii) mlahaka
   iii) wakereketwa .

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

**2. UFUPISHO (alama 15)**

Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu, anayeweza kustahiwa na kusadikikika katika mambo, shughuli na hali tofauti tofauti.

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii. Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa vijulanga wote wanamtegemea kama msimamizi wa mambo nyeti ya maisha yao.

Kwa_hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume na mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, mathalani jukumu ama dhima fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Watu hapana shaka watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo.Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwisha tiwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadilifu daima atajiepusha na shutuma na majanga yote yanayoweza kuchipuka.Kuna msemo maarufu, kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu, kwamba "aliye kando haangukiwi na mti." Pia waliambiwa kwamba,pilipili usiyoila yakuwashiani?

Ni bayana kutokana na misemo hiyo mwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya 'watoro' ambao ni watovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wako mazingirani mwake. Ndipo wa kale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kufikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake. Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote ayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani, watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni kheri mja kujihidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

Maswali

a) Nini umuhimu wa nidhamu? (Maneno kati ya 50 - 55) (alama 1 ya mtiririko) (alama 6)

b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (Tumia maneno 55 - 60) (alama 1 mtiririko) (alama 7)

**3.** MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)

a) Eleza dhana ya shadda. (alama 2)

b) Ainisha viambishi na silabi kwa kutumia kitenzi: (alama 2)
Walipigishwa.

c) Nini wingi wa sentensi hii katika ukubwa? (alama 2)
Ulimi wa mtundu huwa mrefu.

d) Eleza matumizi matatu ya kiimbo. (alama 3)

e) Changanua kwa kutumia mstari / mshale. (alama 4)
Wazazi wengi sana waliofika shuleni mapema walileta vyakula vingi.

f) Yakinisha kwa wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
Hakuwa na kalamu nyeupe.

g) Andika upya sentensi hii ukifuata maagizo. (alama 2)
Wembe ulipopotea mwanafunzi alikasirika. (Anza: Kupotea . . .

h) Toa maana mbili za sentensi hii: (alama 2)
Nionyeshe vile nitakavyokubeba.

i) Kwa kutoa mifano katika sentensi, bainisha matumizi ya kibainishi. (alama 2)

j) Andika katika usemi wa taarifa: (alama 3)
"Mbona unamfanyia karaha mwenzako ? Je, utaenda kumwomba radhi?" Natasha aliuliza.

k) Nomino za ngeli ya A - WA zina sifa gani kimuundo? (alama 2)

l) Bainisha vishazi vilivyotumika katika sentensi hii. (alama 2)
Ingawa alimshtaki hatapata haki.

m) Eleza kazi ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
i) <u>Jumapili</u> ijayo nitakuwa sherehe . . . .
ii) Wageni watakuja <u>Jumapili</u> . . . .

n) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya 'ndi'. (alama 2)

o) Onyesha shamirisho katika sentensi. (alama 3)
Kipkemboi alimbebea mwalimu mzigo kwa gari.

p) Bainisha nomino katika sentensi hii:. (alama 3)
Uhubiri wa Nabii Dkt. David Edwin Owuor una mvuto mkubwa.

q) Tumia 'o' rejeshi mazoea kuandika upya sentensi hii: (alama 2)
Mwanafunzi ambaye anasoma kwa bidii ndiye ambaye anafaulu mtihani

**4. ISIMUJAMII (alama 10)**

a) Eleza sababu sita zinazosababhisha watu kubadili na kuchanganya msimbo (alama 5)

b) Toa ithibati kwamba lugha ya Kiswahili ina asili ya kibantu. (alama 4)

for more free kcse past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call 0720502479